

**TANGAZO LA KAZI
YA
AFISA MAUZO (SAELS EXECUTIVES) – NAFASI 5**

Lalex Industries Company Limited ni Kiwanda kinachozalisha Bidhaa za LALEX kama vile Sabuni, Vipodozi na Tishu iliyosajiliwa tarehe 10 Agosti 2026 Dar Es Salaam – Tanzania na yenye Ofisi Eneo la Makofia, nyuma ya Shule ya Alex Hills (Karibu na Mnara).

Lalex Industries Ltd inatangaza nafasi za Kazi ambapo Waombaji wataanza Majaribio ya Miezi Mitatu (3) huku wakilipwa Posho ya kila Siku, na baada ya miezi mitatu (3) kuna uwezekano wa kuingizwa kwenye mfumo wa ajira ya mkataba wa muda maalum kutokana na makubaliano ya pande zote.

Lalex Industries Ltd itampanga kila Afisa Mauzo kusimamia Wilaya moja (1) ya Mkoa wa Dar Es Salaam.

Afisa Mauzo atawajibika kwa **Sales & Marketing Manager**

Kituo cha Kazi – Dar Es Salaam

Sifa:

- i) Awe na umri Kuanzia miaka 18 na kuendelea
- ii) Awe na Uwezo wa kufanya Mauzo kwa njia ya kawaida (conventional marketing) na mitandao ya kijamii (social media)
- iii) Ujuzi wa kufanya Mauzo ya Bidhaa za Sabuni, Vipodozi na Tishu (Sifa ya Ziada)
- iv) Awe na Simu Janja (Smart Phone)
- v) Uwezo wa Kutumia Kompyuta (sifa ya ziada)
- vi) Kiwango cha Elimu (Uwezo wa Kujieleza, Kushawishi na Kufanya Mauzo)

Kazi na Majukumu:

- i) Kuwa Mwakilishi wa Chapa ya Lalex katika Wilaya atakayopangiwa
- ii) Kutafuta Wateja wa jumla wa bidhaa za Lalex
- iii) Kuandaa taarifa mbalimbali za Mauzo kila siku kwenye muundo wa Kampuni
- iv) Kuwa sehemu ya Timu ya Tafiti ya Masoko
- v) Kutekeleza wajibu mwingine kama atakavyoelekezwa na Msimamizi wake wa karibu

Mwombaji atume Barua ya Maombi na Wasifu wake (CV) kupitia barua pepe (E-mail) iliyooneshwa hapo juu kwenye Logo **bila kuacha nafasi**, na kwa maulizo yoyote tupigie kwa nambari hapo juu.

Mwisho wa kupokea maombi ni Siku ya Jumatatu tarehe 5 Oktoba 2026 Saa 4:30 Asubuhi.

Imetolewa na Mkurugenzi,
Lalex Industries Ltd
S.L.P 75779
Dar Es Salaam

